

STREETNET INTERNATIONAL

# Jukwaa la Kikanda la Afrika la Matakwa Yanayohusu Ulinzi wa Kijamii

# Azimio la StreetNet kuhusu Ulinzi wa Kijamii

Kama ilivyopendekezwa na kuungwa mkono na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa StreetNet katika Kongamano la 7 la Kimataifa, lililofanyika Machi 2023 huko Kigali, Rwanda:

**IKIZINGATIA**

Kwamba ajira na shughuli za uchumi wa sekta isiyo rasmi zimeongezeka kote duniani, na kwamba zaidi ya asilimia 80 ya watu duniani wanategemea shughuli za kiuchumi katika sekta isiyo rasmi, iwe katika maeneo yaliyo pangwa au yasiyo pangwa.

Kutokuwepo kwa usalama, hali duni na hatarishi za kazi, na ukosefu wa upatikanaji wa vifaa sahihi vya kudhibiti hatari ambavyo vinasaidia kupunguza athari za mazingira ya kazi na maisha.

Umuhimu wa ulinzi wa kijamii kwa maisha ya kila raia sasa na siku zijazo, ambao pia unaweza kuboresha uchumi wa dunia.

**IKIANGALIA**

Upendeleo wa serikali katika matumizi ya vyombo vya ulinzi wa kijamii kwa kuwalenga zaidi wafanyakazi wa sekta rasmi, lakini ikitambua mchango wa sekta isiyo rasmi katika uchumi wa kitaifa na kwamba wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi ni wafanyakazi kama wengine.

**PONGEZI**

Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu kuhusu matumizi ya Ulinzi wa Kijamii kwa wote, Kifungu cha 22 na 25 ambacho kinasema yafuatayo:

*Kifungu cha 22*

*Kila mtu, kama mshiriki wa jamii, ana haki ya kupata ulinzi wa kijamii, na ana haki ya kutekelezewa haki hiyo kupitia juhudi za kitaifa na ushirikiano wa kimataifa, kwa mujibu wa mpangilio na rasilimali za kila Taifa, ili kuhakikisha upatikanaji wa haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni ambazo ni muhimu kwa utu wake na kwa ukuaji huru wa utu wake binafsi.*

*Kifungu cha 25*

*Kila mtu ana haki ya kuwa na kiwango cha maisha kinachofaa kwa afya na ustawi wake na wa familia yake, ikiwa ni pamoja na chakula, mavazi, makazi, huduma za afya na huduma muhimu za kijamii, na haki ya kupata usalama wa kijamii iwapo atakumbwa na ukosefu wa ajira, maradhi, ulemavu, ujane, uzee au ukosefu wa kipato kutokana na hali zisizo ndani ya uwezo wake. Wakina mama na watoto wana haki ya kupata huduma na msaada maalum. Watoto wote, waliozaliwa ndani au nje ya ndoa, wanapaswa kupata ulinzi sawa wa kijamii.*

**KWA HIVYO INAAZIMIA**

Kwamba StreetNet ijihusishe na Umoja wa Mataifa, hasa kupitia Shirika la Kimataifa la Kazi (ILO), ili kuhakikisha kwamba Ulinzi wa Kijamii unajumuishwa kikamilifu kwa nchi zote wanachama kwa kuidhinisha na kutekeleza Mkataba wa Hifadhi ya Jamii (Na. 102), Mapendekezo ya Sakafu za Ulinzi wa Kijamii (Na. 202), na Mapendekezo ya Mpito kutoka Sekta Isiyo Rasmi kwenda Sekta Rasmi (Na. 204).

Kwamba kila mshirika wa StreetNet ashawishi na kuiomba serikali yake kupanua mfumo wa Ulinzi wa Kijamii kwa wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi kwa na watapokea msaada wa kitaalamu na misaada mingine muhimu kutoka kwa StreetNet International.

# Madai


## I. Mifumo ya Kisheria

**1.1 Wafanyakazi** – iwe ni waajiriwa au wanaojiajiri – wanapaswa kutambuliwa na kujumuishwa ndani ya mfumo wa sheria za kazi. Mtazamo unapaswa kubadilika kutoka kutegemea uhusiano wa ajira kama msingi wa udhibiti, kuelekea kudhibiti "kazi" na "wafanyakazi". Mifumo ya kisheria inapaswa kufanyiwa mapitio na marekebisho ili kuhakikisha kuwa ulinzi wa kijamii unatolewa kupitia sheria za kazi kwa wafanyakazi wote bila kujali uhusiano wao wa ajira.

**1.2 Serikali** **-** lazima zisaini na kutekeleza mifumo ya kisheria ya kimataifa na kikanda inayohusiana na upanuzi wa ulinzi wa kijamii kwa wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi katika eneo la Afrika, ikijumuisha Mkataba wa ILO Na. 102 kuhusu Hifadhi ya Jamii (Viwango vya Chini), Mapendekezo ya ILO Na. 204 kuhusu Mpito kutoka Sekta Isiyo Rasmi hadi Rasmi, na Itifaki ya Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu kuhusu Haki ya Wananchi kwa Ulinzi wa Kijamii na Hifadhi ya Jamii.

**1.3 Marekebisho** - yasiishie kuwa uhakika wa kisheria pekee. Mabadiliko kuelekea sheria zinazounga mkono zaidi yanapaswa kuambatana na mipango halisi na inayotekelezeka, inayojumuisha ushiriki wa wawakilishi wa mashirika ya wanachama ya wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi.

*Soko mjini Accra, Ghana, 2022. Picha na StreetNet Media.*



# 2. Ufadhili wa Ulinzi wa Kijamii

2.1 Ufadhili wa ulinzi wa kijamii unapaswa kuzingatia **misingi ya mshikamano** – kila mtu achangie kulingana na uwezo wake, na kila mmoja apokee kulingana na mahitaji yake; wale wanaopata kipato kikubwa zaidi katika jamii wanapaswa kuchangia zaidi ili kusaidia wale wasio na uwezo mkubwa wa kuchangia.

2.2 Bajeti za serikali lazima zijumuishe **malengo mahususi ya matumizi katika mipango ya ulinzi wa kijamii** inayojumuisha wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi, ili kuongeza kiwango cha manufaa kwa wafanyakazi wote.

2.3 Ili kuhakikisha upatikanaji wa fedha za kutosha kwa ajili ya ulinzi wa kijamii, **msingi wa ushuru lazima uimarishwe kupitia mifumo ya ushuru inayoongezeka kwa haki bila kuweka mzigo mkubwa wa kodi kwa wafanyakazi maskini wa sekta isiyo rasmi.** Hii ni pamoja na, lakini siyo tu, hatua kama kuongeza ushuru kwa bidhaa hatarishi (kama vile pombe na tumbaku), bidhaa za anasa, ushuru wa utajiri, kujumuisha ulinzi wa kijamii katika mikakati ya mabadiliko ya tabianchi na upunguzaji wa hatari za majanga, kukomesha mifumo haramu ya mtiririko wa fedha, na kuhakikisha ushuru wa makampuni ni wa haki na unaolingana.

2.4 **Kodi za ziada au ongezeko la kodi ambazo zinaweza kuwaathiri wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi, hasa wale maskini, zinapaswa kujadiliwa na wawakilishi wa mashirika ya wanachama kabla ya utekelezaji. Hatua hizo zinapaswa kubuniwa kwa uangalifu ili kupunguza athari kandamizi**. Ongezeko la kodi ya matumizi kama vile Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) halipaswi kujumuisha bidhaa na huduma za msingi, na ushuru wa miamala ya kidijitali unapaswa kulenga miamala mikubwa pekee.

2.5 Mipango ya ulinzi wa kijamii inayohusisha michango ya moja kwa moja **inapaswa kuweka viwango halisi vya michango vinavyoendana na mapato ya sekta isiyo rasmi.** Kutambua utofauti wa sekta isiyo rasmi, viwango vya michango vinapaswa kuwa vya kubadilika ili kuruhusu michango mikubwa au midogo kulingana na hali ya kipato. Njia kama ruzuku na michango inayolinganishwa zinapaswa kuwepo ili kuhakikisha kwamba wafanyakazi maskini hasa wanawake, ambao hutumia muda nje ya soko la ajira kutokana na majukumu ya malezi, wanapata manufaa ya kutosha licha ya michango yao kuwa midogo au kukatika.

2.6 Mfumo kama Mfuko wa Kimataifa wa Ulinzi wa Kijamii (Global Social Protection Fund) unapaswa kufadhiliwa vya kutosha na nchi wanachama wa OECD **ili kuwezesha mgawanyo wa rasilimali kwa usawa duniani kote, kwani ufadhili unaotegemea mgawanyo wa rasilimali ni muhimu kwa usawa wa ndani ya nchi na baina ya nchi.**

2.7 **Ufadhili wa mshikamano wa kimataifa** unapaswa kuendelezwa kama nyenzo muhimu ya kuhakikisha kuwa nchi maskini zina uwezo wa kueneza ulinzi wa kijamii kwa ufanisi zaidi.

## 3. Usimamizi wa Mipango ya Ulinzi wa Kijamii

3.1 **Majadiliano ya kijamii yanapaswa kuwa msingi wa mageuzi yote ya ulinzi wa kijamii** na lazima yajumuishe moja kwa moja wawakilishi wa mashirika ya wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi, ikiwemo mashirika ya wafanyakazi wanaojiajiri katika sekta isiyo rasmi.

3.2 **Wawakilishi wa wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi kutoka sekta mbalimbali wanapaswa kushirikishwa katika kila hatua ya mchakato wa kuandaa na kutekeleza mipango ya ulinzi wa kijamii**. Lazima washauriwe katika hatua ya kubuni mpango, wapewe nafasi katika uongozi wa mpango, na wahusishwe kikamilifu wakati wa utekelezaji. Kanuni ya "Hakuna kilicho chetu bila sisi wenyewe" lazima izingatiwe.

3.3 U**simamizi wa mipango ya ulinzi wa kijamii lazima uwe wa kitaalamu, uwajibikaji na uwazi.** Kwa mipango inayohitaji michango ya moja kwa moja, wafanyakazi wanapaswa kuwa na haki ya kupata taarifa zote kuhusu michango yao. Mfumo wa kupokea maoni na mrejesho ambao ni rahisi kufikika na kufanya kazi ipasavyo, lazima ujumuishwe katika mpango ili wafanyakazi wote waweze kuwasiliana na maafisa wa mpango kuhusu masuala yao.

3.4 Mipango ya ulinzi wa kijamii inayolenga wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi inapaswa **kusimamiwa kupitia majukwaa ya uratibu ya wizara mbalimbali, ambayo yanahakikisha kuwa wizara zenye nguvu na zile dhaifu zinafanya kazi kwa pamoja.**

## 4. Ubunifu wa Mipango ya Ulinzi wa Kijamii

4.1 Mipango ya ulinzi wa kijamii inayotegemea michango inapaswa kutumia **mifumo ya michango inayopanda kwa hatua (graduated models) ili kutoa unyumbufu katika kiasi na muda wa kuchangia.**

4.2 Masharti ya kiutawala ya mipango yote ya ulinzi wa kijamii, iwe ya kuchangia au isiyo ya kuchangia, yanapaswa kurahisishwa **ili kurahisisha mchakato wa usajili, uchangiaji, na upokeaji wa mafao.**

4.3 **Vifaa vya kidijitali** vinapaswa kutumika kurahisisha malipo ya michango na upokeaji wa mafao. Hata hivyo, **vifaa hivi lazima viwe rafiki kwa mtumiaji, jumuishi, na vifikike kwa kila mtu**; njia za kawaida (zisizo za kidijitali) zinapaswa kuwepo na msaada wa ziada utolewe kwa wale wanaohitaji msaada kutumia vifaa vya kidijitali.

4.4 Mafao yanapaswa kubuniwa ili kushughulikia **vipaumbele vya haraka na vya muda mrefu vya wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi**, hata kama mafao hayo yako nje ya tafsiri ya kawaida ya ulinzi wa kijamii. Lazima yashughulikie mahitaji maalum ya wanawake wanaofanya kazi katika sekta isiyo rasmi, ikiwa ni pamoja na mafao ya uzazi na upatikanaji wa huduma za kulea watoto.

4.5 Malipo ya mafao lazima yafanyike kwa **wakati na kwa uthabiti.** Hili litawezesha kujengwa kwa uaminifu kati ya wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi na mfumo wa ulinzi wa kijamii.

4.6 Mipango ya ulinzi wa kijamii inapaswa kubuniwa kwa njia ambayo **inaimarisha ushirikiano na uundaji wa vyama kati ya wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi.** Hili linaweza kufanikishwa kwa njia mbalimbali kulingana na muktadha, ikiwa ni pamoja na kuimarisha uhusiano na mipango ya uchumi wa kijamii na mshikamano inayotengenezwa na mashirika ya wafanyakazi.

## 5. Utekelezaji wa mifumo ya ulinzi wa jamii

5.1 Utekelezaji madhubuti na wa kweli wa mipango ya ulinzi wa kijamii lazima uwe kipaumbele, **ukiwa na mipango ya wazi ya utekelezaji iliyoandaliwa kikamilifu na kushirikishwa kwa mashirika ya wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi.**

5.2 **Mipango ya utekelezaji inapaswa kuandaliwa kwa njia shirikishi**, na kwa kutambua jukumu muhimu la mashirika ya wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi katika kuelimisha jamii, rasilimali za kutosha zinapaswa kutengwa ili kusaidia kazi hiyo.

5.3 Mipango ya utekelezaji lazima ijumuishwe **na mkakati wazi wa mawasiliano pamoja na ufadhili kwa ajili ya utekelezaji wake, ili kuhakikisha kuwa wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi wanaelewa mpango**, umuhimu wake na jinsi ya kuufikia. Taarifa hizi zinapaswa kutolewa kwa lugha za kienyeji kupitia vyombo vya habari vinavyofikika kwa wafanyakazi wote.

5.4 **Mkakati wa wazi ya ufuatiliaji na tathmini lazima iwepo ili kuhakikisha kuwa malengo yanatimizwa**, na changamoto zozote katika utekelezaji wa mipango ya ulinzi wa kijamii zinakusanywa na kushughulikiwa. Hii inapaswa kujumuisha mapitio ya mara kwa mara ya mpango ili kuendana na mwelekeo na hali halisi ya sasa.

*Muuzaji chakula mjini Dakar, 2022. Picha na Marta Moreiras*



# Matarajio ya Wadau

Kwa kutambua kwamba Serikali ndiyo yenye jukumu la mwisho la kutoa ulinzi wa kijamii na kuwezesha michakato shirikishi ya kutekeleza suala hilo, **wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi wanatoa wito kwa wadau wengine muhimu kushiriki katika kuwezesha upatikanaji wa ulinzi wa kijamii kwa wafanyakazi WOTE**. Wadau hao ni pamoja na:

## A. Vyama vya Wafanyakazi

A.1 Vyama vya wafanyakazi vinapaswa kujitahidi **kujumuisha mashirika ya kidemokrasia ya wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi, ikiwemo katika ngazi ya mashirikisho ya vyama vya wafanyakazi ya kikanda**. Katiba za vyama vya wafanyakazi zinapaswa kufanyiwa marekebisho ili kuruhusu uanachama kamili wa mashirika ya wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi.

A.2 Vyama vya wafanyakazi vina jukumu muhimu la **kujenga uwezo wa wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi kushiriki katika mazungumzo ya pamoja na utetezi kwa ajili ya kuboresha ulinzi wa kijamii.** Hii inajumuisha utafiti wa sera, mafunzo na elimu kuhusu uendeshaji wa mashirika ya kidemokrasia, mikakati ya kuandaa wanachama, ulinzi wa kijamii na wa kazi, kufungua fursa za kujenga miungano na wadau muhimu wa ulinzi wa kijamii ndani na nje ya vuguvugu la wafanyakazi, na kukuza madai ya wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi.

A.3 Vyama vya wafanyakazi vinapaswa **kuunga mkono kwa dhati ushirikishwaji wa moja kwa moja wa wawakilishi wa wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi katika majadiliano ya kijamii, hasa pale ambapo mashirika hayo tayari yamejiunga kama wanachama kamili.** Wawakilishi wa wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi pia wanapaswa kuwakilishwa katika vyombo vyote muhimu vya kufanya maamuzi ndani ya vyama hivyo.

## B. Mashirika ya Kiraia

B.1 Mashirika ya kiraia yanapaswa kuunda **mazingira ya ushirikiano kwa ajili ya miungano ya ulinzi wa kijamii, kwa kutumia nguvu na uwezo tofauti wa mashirika mbalimbali.** Mashirika ya wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi lazima yajumuiwe katika miungano hiyo.

B.2 Mashirika ya kiraia yanaweza **kutumia utaalamu wao kuchangia katika shughuli za utetezi, mitandao, utafiti, na ujenzi wa ushirikiano ili kusaidia uhamasishaji wa rasilimali,** na kushirikiana taarifa hizo na mashirika ya wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi.

## C. Mashirika ya Wafanyakazi Wa Sekta Isiyo Rasmi

C.1 Ni jukumu la mashirika ya wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi kuunda **mkakati na ajenda madhubuti kuhusu ulinzi wa kijamii na kuhakikisha wanachama wao wanauelewa na kuuunga mkono**. Hii inajumuisha kuelimisha na kuhamasisha ulinzi wa kijamii, ikiwa ni pamoja na kutumia kwa ubunifu njia mbalimbali za vyombo vya habari.

C.2 Mashirika ya wafanyakazi wa sekta isiyo rasm**i lazima yajenge mashirika yenye wanachama hai na waliodhamiria, kwa kukuza maadili ya utawala bora na uwazi katika uendeshaji wa mashirika yao.** Pia yanapaswa kujitahidi kuendeleza huduma kwa wanachama wao, ikiwa ni pamoja na huduma za akiba, ulinzi wa kijamii, na huduma zingine muhimu.

C.3 Mashirika ya wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi yanapaswa **kuwa tayari kushiriki kikamilifu kama wadau hai katika miungano na majukwaa yaliyopo yanayojitolea kukuza ulinzi wa kijamii jumuishi katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa.** Hii ni pamoja na kushiriki katika shughuli za kielimu, kujifunza jinsi ya kushirikiana kwa ufanisi na viongozi wa serikali waliochaguliwa, na kujifunza kuchambua bajeti ili kutoa hoja ya kifedha kuhusu upanuzi wa ulinzi wa kijamii.

# Wachangiaji

1. Zimbabwe Chamber of Informal Economy Associations (ZCIEA) Zimbabwe
2. Alliance for Zambia Informal Economy Associations (AZIEA) Zambia
3. Association of Vendors and Marketeers in Zambia (AVEMA) Zambia
4. Rwanda's Trade Union for Domestic and Independent Workers in the Informal Economy (SYTRIECI) Rwanda
5. Faitiere Nationale des Travailleurs du Secteur Informelle (FAINATRASIT) Togo
6. Federation of Informal workers organisation of Nigeria (FIWON) Nigeria
7. Confédération National des Travailleurs du Sénégal (CNTS) Sénégal
8. Kenya National Alliance of Street Vendors and Informal Traders (KENASVIT) Kenya
9. Sierra Leone Traders Union (SLeTU) Sierra Leone
10. Tanzania Union of Industrial and Commercial Workers (TUICO) Tanzania
11. Union Syndicale des Vendeuses et Vendeurs de Pièces Détachées et Divers du Marché de Dantokpa (UNSYNVEPID-CSPIB) Bénin

**Tunawashukuru pia wataalamu wa kiufundi kutoka Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Wafanyakazi – Afrika (ITUC-Africa), Jukwaa la Afrika la Ulinzi wa Kijamii (APSP), na Wanawake katika Ajira Isiyo Rasmi: Utandawazi na Uratibu, ambao walichangia katika kuandaa jukwaa hili la madai.**

media@streetnet.org.za

+351 938 291 185

www.streetnet.org.za

@StreetNetInternational

@street_net_international

@Streetnet1